

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

MAOMBI YA KUPIGIWA KURA KWA MIRADI YA TEHAMA ILIOCHAGULIWA KUSHINDANISHWA KWENYE TUZO ZA WSIS 2024

Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa kushirikiana na Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) na waratibu wake wameandaa mkutano wa kilele wa WSIS kwa mwaka 2024. WSIS ni mfululizo wa mikutano inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa, ikiwa na lengo la kujadiliana kuhusu fursa na changamoto zinazoletwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika karne hii ya sasa.

Kwa kurejelea Taarifa kwa Umma iliyotolewa tarehe 29 Novemba 2023, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mwanachama wa ITU inashiriki katika Tuzo za WSIS 2024 na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kama mratibu inawashukuru wadau wote waliowasilisha miradi yao. Aidha TCRA inayo furaha kuujulisha umma na wadau wa WSIS kuwa miradi mitano (5) kutoka Tanzania imechaguliwa kwa hatua ya kupigiwa kura. Hii ni hatua muhimu inayoonyesha mchango wa Tanzania katika kutumia TEHAMA kwa maendeleo chanya. Siku ya mwisho ya kupiga kura ni Machi 31, 2024.

Orodha ya miradi iliyochanguliwa kutoka Tanzania kwa Tuzo za WSIS 2024

S/N	Jina la Mradi	Taasisi
1	Mradi wa CSA - Kituo cha Huduma Jumuishi	Shirika la Tech & Media Convergency (TMC)
2	Mradi wa Ujenzi wa Minara ya Simu Zanzibar	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)
3	Mradi wa Ushirikishwaji wa Kidijitali Tanzania	Shirika la Organisation for Digital Africa
4	Shindano la Cyber Champions	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
5	Mradi wa Matumizi ya ufuatiliaji wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha ugunduzi wa mapema	Wizara ya Afya

TCRA inawahimiza Umma kwa ujumla na zikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, taasisi za kimataifa na kikanda, asasi za kiraia na wanataaluma kupigia kura miradi hii kabla au kufikia Machi 31, 2024 ili kuipa nafasi miradi ya Tanzania kushinda tuzo hizi za muhimu.

Taratibu za Kupiga Kura: kupiga Kura tumia kiunganishi hiki
<https://www.itu.int/net4/wsis/stocktaking/Prizes/Prizes/> kujisajili kwenye Jukwaa la WSIS chini ya Tuzo za WSIS 2024 kisha kufuata maelekezo na kupiga kura.

Tafadhali Kumbuka masharti ya fuatayo: Kila mwanachama anaweza kupiga kura/kuunga mkono mradi mmoja tu katika kila kategoria/mstari wa hatua, na pia, Taasisi haziruhusiwi kupiga kura/kuunga mkono mradi wao wenyewe. **Ukomo wa kupiga kura ni tarehe 31 Machi 2024.**

Imetolewa tarehe 20 Machi, 2024.


John Daffa
KAIMU MKURUGENZI MKUU

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tora.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz